# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

# SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI

# S.L.P. 100, MAHENGE/ULANGA.

**NAMBA ZA SIMU:**

**Mkuu wa Shule: 0655883770/0784893770.**

**Makamu wa Mkuu wa Shule: 0684744774**

**Matron/Patron: 0685720269/0712036539.**

**Tarehe 26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2024/2025.

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024/2025** na atasoma tahasusi ya HGL/HGLi/CBG.

Shule ya Sekondari **CELINA KOMBANI** ipo umbali wa Kilometa 43 Kusini-Mashari mwa Mji wa **MAHENGE** Usafiri wa basi kutoka mjini **MAHENGE** unapatikana katika kituo cha mabasi **MAHENGE** Nauli ni Shilingi 7,000.00 kwa basi hadi Mwaya mjini na kutoka Mwaya mjini ni shilingi 1,000.00 kwa pikipiki na Shilingi 1,000.00 kwa bajaji hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30**/06/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe 13/07/2024.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1. Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni **Sketi mbili** iwe ya mshono wa linda box mbele na nyuma (**ndefu ambayo huachia inchi sita tu** (**pima hizo nchi sita ukianzia usawa wa ardhi**), rangi "nyeusi"(cotton) kwa Wasichana na **suruali mbili** ya kawaida rangi "nyeusi"(cotton (**iwe na seleburesheni na turn-up na upana wa mguu wa suruali kwa chini iwe inchi 16)- TAFADHALI NAOMBA ZINGATIA SANA VIPIMO**.

ii. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu (tomato) lisilobana mwili (kwa wasichana na wavulana)

iii. Rangi ya Hijab (juba) ni ya darasani yenye rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni track suit mbili za **rangi ya njano na viatu aina ya raba** kwa ajili ya michezo Kwa wasichana na track suit mbili za **rangi ya light blue na viatu aina ya raba** kwa ajili ya michezo kwa wavulana.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na Soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana za shule

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.

viii. Sweta 02 za bluu **– yenye umbo la V shingoni.**

ix. Nguo za kushindia **(shamba dress)** sketi 02 za rangi ya kijivu ndefu mpaka chini iwe ya mshono wa linda box mbele na nyuma kwa wasichana na suruali 02 za kijivu kwa wavulana (**iwe na seleburesheni na turn-up na upana wa mguu wa suruali kwa chini iwe inchi 16**.

x. Tai mbili za rangi nyeusi na mistari myeupe zenye nembo ya shule zitapatikana shuleni kila moja kwa gharama ya 8,000/=

xi.Tisheti (T-shirt) 02 za rangi ya njano za kushindia baada ya masomo yenye kola na T-Shirt 02 za rangi ya kijivu za darasani zinavaliwa siku maalumu katika wiki yenye kola na yenye nembo ya shule zitapatikana shuleni, kila moja kwa gharama ya 15,000/=

**ANGALIZO**: **Ni marufuku mwanafunzi kuja na nguo/ sare ambazo hazikuelekezwa katika fomu hii.**

### 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Daftari saba counter book quire 3 au 4 na Daftari 10 ndogo kwa ajili ya majaribio ya mwezi.

ii. **Ream ($A_4$)** ya Karatasi Mbili (02) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology.
v. Scientific Calculator.
vi. Godoro moja 2.5” x 6”
vii. Mashuka Jozi 2 (za rangi ya pinki kwa wasichana na light blue kwa wavulana.), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*cheupe)*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe-vyote viwe vya udongo/mfupa na siyo plastiki nyepesi)
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
xii. Vifaa vya usafi (squeezer rubber na mpini 01, mop complete 01, dawa ya chooni 01, toilet brush 01 na hard bloom 01)

***Angalizo: usije na fedha badala ya kifaa kilichotajwa hapo juu (lete kifaa husika)***

## 2.1 MICHANGO MBALIMBALI

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Zingatia: Fedha zote ziwekwe kwenye Benk ya NMB,**
**JINA LA AKAUNTI: SELINA KOMBANI SECONDARY SCHOOL,**
**NAMBA YA AKAUNTI: 21901100009, katika tawi lolote la NMB. Mwanafunzi ajapo shuleni aje na *"Bank Pay in Slip".* Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye Pay slip. hakuna pesa itakayopokelewa mkononi.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi

yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma adhabu halali na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi,ear/head phone, sim card katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa au wimbo wa shule.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**ULANGA DISTRICT COUNCIL - MOROGORO**

**CELINA KOMBANI SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**(Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali)**

To be completed by medical Officer in respect of CELINA KOMBANI Secondary School Student (Entrant).

1. Full name of student………………………………………………………………………..
2. Sex………………………………Age ……………………………………… .
3. HB Test…………………………... .
4. Stool……………………………………… .
5. Urine Micro……………………………….

6. T.B Test…………………………..

7. Eye Examination………………………..

8. E.N.T…………………………….

9. Chest………………………………

10. Abdomen……………………………

ADDITIONAL INFORMATION

Physical Defects or Impairment, Infections, Chronic or Hereditary (family) diseases

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above student and consider that* he/she is physically/not physically fit for further studies.

NAME………………………………………………SIGNA TURE………………………………………

DATE ………………………………………………………..

……………………………………………………..

OFFICIAL STAMP.

**SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI. FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI.**

Ndugu Mzazi/ Mlezi, Shule inahitaji kufahamu mambo yafuatayo kuhusu mtoto wako.

Jina kamili la mwanafunzi ………………………………………………………………...

- Tarehe yake ya kuzaliwa ……………………………………………………………
- Shule ya sekondari atokayo (o-level)……………………………………………..
- Wilaya……………………………………………………………………………………..
- Mkoa……………………………………………………………………………………
- Taifa……………………………………………………………………………………
- Kabila lake ……………………………………………………………………..
- Dini yake ……………………………………………………………………….
- Je, ana ugonjwa wowote unaomsumbua mara kwa mara? **NDIYO/HAPANA** Kama ndiyo anatibiwa hospitali gani? ……………………………………………………………
- Anaishi na nani akiwa nyumbani , Mzazi/ Mlezi …………………………………….
- Jina la mzazi/ mlezi …………………………………………………………….
- Anuani yake ………………………………………………………………………
- Simu ya mkononi/ nyumbani ……………………………………………………..
- Simu ya kazini …………………………………………………………………...
- Kazi ya mzazi/ mlezi ……………………………………………………………..
- Sehemu unakoishi kwa sasa ……………………………………………………..

**IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI.**

Mimi …………………………………….. **NINAKUBALI/ SIKUBALI** Nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari Celina Kombani. Naahidi kukubaliana na sheria za shule na kumtimizia mahitaji yote mwanangu kabla ya kujiunga na Shule na maelekezo mengine sahihi yatakayotolewa na shule kwa mujibu wa sheria ya uendeshaji wa Shule nchini Tanzania.

SAHIHI…………………………………………………………………...TAREHE …………………SIMU……………………

**IJAZWE NA MWANAFUNZI HUSIKA.**

Mimi ………………………………………………………….. **NINAKUBALI/ SIKUBALI** nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Celina Kombani. Naahidi kukubaliana na sheria za shule na kutunza mali za shule na maelekezo mengine sahihi nitakayopewa na shule. Na sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

SAHIHI ……………………………………………………………………...TAREHE ……………………………………..

**ASANTE KWA USHIRIKIANO MWEMA**

**PAUL KAJURUNGA JOHN**

**MKUU WA SHULE.**

i. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi w

anaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI**

**PAUL KAJURUNGA JOHN**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0655883770/0784893770**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0684744774**
- **Mwandamizi Taaluma : 0692996015.**
- **Mwandamizi Malezi : 0782377711.**

**A- LEVEL BOOKS REQUIREMENTS**

**GEOGRAPHY PARER 1**

1. Principles of physical Geography – by F.J Monkhouse
2. A comprehensive approach to physical Geography for secondary school – by D.T Msabila
3. Practical Geography for Africa By John M. Prichard
4. Land forms in Africa – an introduction to Geomorphology – by Colin Buckle
5. Africa – by J.M Prichard
6. Practical Geography for A level – by Francis Mnyawi
7. An integrated approach to Geography – by David Waugh

**GEOGRAPH PAPER II**

1. Human and Economic Geography – by Goh Cheng & Morgan

2. Advanced level geography Course book – by Tanzania Institute of Education (TIE)

3. An integrated focal regional study on human and Economic Geography Advanced level paper by D. T Msabil

**ENGLSH LANGUAGE 1**

1. A practical approac

h by Asheli, N.E

2. An introduction to Language Advanced level by. Kadeghe, M

**ENGLISH LANGUAGE 2**

**A: NOVELS AND SHORT STORIES**

1. A man of the people by Chinua Achebe
2. The beautiful ones are not yet Born by. Ayi Ewei Armah
3. His Excellency the head of state by Sago

**B: PLAYS**

1. I will marry when I want by NNgugi wa Thiong'o & Ngugi wa Murrii
2. An enemy of the people by. H.Ibsen
3. The Causasian Chalk Circle by. B.Bretch
4. Betrayal in the City by. F.Imbuga
5. Not yet Uhuru
6. Rwanda Magere
7. Black Mamba

C. **POETRY:**

1. Tanzania institute of Education: selected poems
2. David Cook et. Al: poems from East Africa

**HISTORY:**

(i) How Europe underdeveloped Africa: Nairobi Heinemann Kenya (1992) by. Rodney w

(ii) Africa in world History A- Level Certificate Notes DSM (DUP) 1992. By Nyirenda H. D

**BIOLOGY**

1. Biological Science
2. Understanding Biology

**CHEMISTRY**

1. Advanced Chemistry by Ramsdem
2. Inorganic Chemistry Part I na Part 2 (TIE)
3. Chemistry for Secondary Schools FY, FYI by TIE

**GENERAL STUDIES**

1. General Studies for Advanced Level Certificates Form
2. Understanding General Studies for Advanced level. by Joannes Bigirwamungu &Sospeter M. Deogratius

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics (BAM) for Advanced level Secondary

SARE NYEUSI COTTON

SARE YA KIJIVU

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI**



**PAUL KAJURUNGA JOHN**

HEAD OF SCHOOL
CELINA KOMBANI SECONDARY SCH
P.O. BOX 100
MAHENGE/ULANGA